

Jifunze kuhusu watoto wa Baba
wa Mbinguni ulimwenguni kote.

Salamu kutoka PAPUA NEW GUINEA!

Papua New Guinea ni nchi ya kisiwa katika Bahari ya Pasifiki. Inachukua nusu
ya kisiwa cha New Guinea. Zaidi ya watu milioni 8 wanaishi huko.

MAKANISA

Mafuriko hutokea kila mara
huko Papua New Guinea. Kwa
hiyo majengo ya kanisa huko
yanajengwa juu ya nguzo.
Wakati mafuriko yanapokuja,
waumini wanaweza kutumia
mitumbwi yao kufika mlangoni
mwa kanisa!



NDEGE WA MSITUNI

Ndege wa paradiso ni ndege wa
msituni wenye haya. Ndege wa
kiume wana mabawa mazuri
yenye rangi nyingi. Ndege wa
Raggiana wa paradiso yuko
kwenye bendera ya nchi.

Yu stap gut?

Hiyo inamaanisha
"Habari yako?" kwa
Kitok Pisini!

IMBA-IMBA

Makabila katika Papua New
Guinea hukushanyika kuimba,
kucheza dansi, kushiriki tamaduni
na kufanya urafiki. Zaidi ya
makabila 100 huunganika
kwenye imba-imba kila mwaka!

LUGHA

Papua New Guinea ina
lugha nyingi zaidi ya nchi
yoyote ulimwenguni—
karibia lugha 840!

VIELELEZO NA ZHEN LIU



SHUGHULI

Vipepeo Wakubwa Sana

Papua New Guinea ina aina kubwa sana ya kipepeo! Tengeneza
kipepeo wako mwenyewe. Kusanya vijiti, majani na maua ili
kuunda umbo. Tumia rula upande wa kulia ili kuona jinsi saizi ya
mabawa ya kipepeo wako yanavyolingana.

Upana wa mabawa ya kipepeo aitwaye Queen Alexandara:
sentimita 28 (nchi 11)

MAELEZO
YA UPISHI

Chungu cha Kuku

Haya ndiyo maelezo ya upishi huko Papua New Guinea. Hili
ni toleo unaloweza kujaribu!

1. Weka **ratili 2 1/2** (kilo 1) kuku aliyekatakwatwa kwenye
chungu na ongeza **mafuta ya kupikia 1/2 kijiko cha
mezani**. Ongeza **kijiko 1 cha kila binzari** na **kijiko 1 cha
chumvi**.
2. Katakata **kiazi kitamu 1** (au mboga za chaguo lako)
na **fungu 1 la vitungu vya kijani**. Ongeza chunguni
kikombe 1 cha mahindi.
3. Weka **tui la nazi 1/2 kikombe** juu ya mboga na nyama.
Funika chungu na uache ichemke kwa moto kidogo.
Chemsha pole pole kwa dakika 30–40.

Hakikisha unapata msaada wa mtu mzima!